



RABIUL THANI 1448 HIJIRIA - OKTOBA 2026 MILADIA (Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

KUKOSEKANA KWA AMANI DUNIANI: UBEPARI NDIYO

CHANZO



Tarehe 20, Septemba ya kila mwaka huadhimishwa kuwa Siku ya Amani Duniani. Mabepari baada ya kushindwa kuleta amani, usalama, utulivu na ustawi wa ulimwengu wakabuni siku ya kuwarubuni watu kuhusu suala la amani ya ulimwengu, huku wao wakiwa ndiyo chanzo na wahusika wakubwa wa upotevu wake. Mfumo wa kibepari ulianza takriban kuanzia karne ya 12 CE hivi ukitokamana na mfumo wa kiujima (feudalism) katika Ulaya ya Magharibi, hii ilisababishwa na maendeleo ya uvumbuzi wa mashine mbalimbali. Uliendelea kukua mfumo huo ukitumia ukoloni kama mbinu yake kuu ya kufikia malengo yake ambayo ni unyonyaji.

Ubepari unaamini katika kutenganisha dini na maisha (usekula) na kipimo cha maslahi. Mambo mawili hayo ndio huzingatiwa katika

nidhamu zake zote za kimaisha iwe siasa, jamii, uchumi nk. Wakaathirika mabepari na mitazamo hiyo na wakasonga mbele katika kuifanyia kazi na hatimaye kwa fikra hizo wakakoloni dunia nzima katika karne ya 19 CE

Kwavile lengo la ubepari na mabepari ni maslahi, kwa kupitia unyonyaji na ukoloni wameleta madhara makubwa yasiyomithilika katika uso wa ulimwengu, na kubwa zaidi ni la ukosefu wa amani.

Tangu uvamizi na uporaji wao ulipoanza sehemu mbali mbali, matokeo yake ulipingwa na watu wote duniani. Kupitia biashara ya utumwa pekee waliyofanya kuanzia karne ya 15 CE, zaidi ya watu milioni 180 waliuawa wengi wao wakitokea Afrika. Si hayo tu bali ubepari kwa kupitia ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo umeleta na unaendelea kuleta vita na machafuko mengi duniani. Kuanzia mwishoni mwa karne ya 19 CE

Inaendelea ...Uk. 3

Yaliyomo :

- ♦ Uganda inapaswa kukabiliana na adui halisi, si kuwafukuza Waturuki.....2
- ♦ Kudhamini deni pamoja na fidia.....4
- ♦ Tunachojifunza kutokana na Khilafah ya Bani Ummayyah.....5
- ♦ Usaliti wa raisi Saadat katika makubaliano ya Camp David.....7

UBEPARI UMESHINDWA

HATA KATIKA SUALA

MAKAZI BORA



Kila mwaka siku Jumatatu ya kwanza ya mwezi wa Kumi, yaani mwezi wa Oktoba, dunia huazimisha Siku ya Makazi Duniani (World Habitat Day). Maadhimisho haya yana malengo kadhaa ikiwemo kuhamasisha kuhusu Makazi bora, salama na yenye gharama nafuu, kuhamasisha upangaji wa Miji na makazi endelevu, kujadili na kutatua changamoto za ukuaji wa miji na makazi yasiyo rasmi, na kuhamasisha Haki ya kila mtu kupata makazi bora.

Kwa mujibu wa Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-Habitat), licha ya juhudi zote na maadhimisho haya ya kila mwaka, bado Dunia inakabiliwa na tatizo kubwa makazi ya binadamu, ambapo zaidi ya watu bilioni 3 hawana makazi yanayofaa, salama au yenye uhakika, na zaidi ya watu bilioni 1 wanaishi katika makazi duni kabisa yasiyo rasmi au mitaa ya mabanda.

Inaendelea Uk. 3

UGANDA INAPASWA KUKABILIANA NA ADUI HALISI, SI KUWAFUKUZA WATURUKI

Tarehe 9 Septemba 2026, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Uganda (CDF), Jenerali Muhoozi Kainerugaba, ambaye ni Mtoto wa Rais wa Uganda Yoweri Museveni, alitoa agizo kupitia akaunti zake rasmi za mitandao ya kijamii kuwa raia wote wa Uturuki waondoke nchini Uganda mara moja na maandamano ya kushinikiza utekelezaji wa agizo hilo yamepangwa kufanyika katika Ubalozi wa Uturuki tarehe 18 Septemba 2026.

Tamko la Jenerali Muhoozi kwa kiasi fulani linahusishwa na mzozo kuhusu Mkosoaji wa serikali ya Uganda na Mwanablogu maarufu Fred Lumbuye, ambaye kwa sasa anaishi nchini Uturuki ambapo hapo awali, serikali ya Uganda imekuwa ikiitaka mamlaka za nchini Uturuki kumkabidhi Lumbuye kwa Uganda au kumfukuza nchini humo.

Kampeni hii mbaya, ovu isiyostahili ya kuwachafua na kuwashambulia Waturuki nchini Uganda inaonekana kufikia hatua mbaya, licha ya ukweli kwamba serikali ya Uganda imekuwa ikinufaika na Uturuki na kuwa na uhusiano mzuri na Uturuki kwa miaka mingi katika sekta mbalimbali, ikiwemo biashara, miundombinu, elimu, viwandani na utalii.

Kinachoonekana katika kampeni hii ya Uganda dhidi ya Uturuki ni zao la chuki na hofu ya serikali ya Museveni dhidi ya Uislamu, ambayo ni athari na sehemu ya kampeni ovu za nchi za Magharibi dhidi



ya Uislamu na Waislamu.

Kupitia kampeni hiyo ya nchi za Kikoloni za Magharibi, Uganda imeweka wazi uungaji mkono wake kwa Kijidola haramu cha Kiyahudi (Israel) katika hatua zake za kijeshi huko Gaza, ambazo zimekosolewa na kulaaniwa kimataifa na pia Uganda imetangaza nia ya kutuma wanjeshi wake Gaza kwa kile kinachoitwa operesheni ya kulin-da amani; jambo ambalo kihalisia ni hatua ya kuisaidia Israel katika juhudi za kuwadhibiti na kuwaua Waislamu wa Palestina. Vilevile, Jenerali Muhoozi ametoa mara kadhaa kauli za wazi za kuunga mkono mashambulizi ya Marekani dhidi ya Iran. Kwahiyo kati ya Uturuki na Marekani, pamoja na Kambi yake ya Kijeshi (Israel) ni nani anastahili zaidi kufukuzwa nchini Uganda?

Bila hata kutaja vitendo vya kikatili vinavyofanywa na Uganda dhidi ya Waislamu na Uislamu kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi kwa shinikizo la Marekani, vitendo ambavyo hazijaweza kuzuia ukuaji wa Uislamu nchini Uganda badala yake, idadi ya Waislamu imeongezeka kutoka takribani milioni 4.66 mwaka 2014 hadi milioni 6.05 mwaka 2024.

Uislamu ulifika Uganda mapema, wakati wa enzi za Ufalme wa Buganda, kupitia pwani ya Afrika Mashariki.

Walinganizi wa Kiislamu na Wafanyabiashara hasa Waarabu, wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki, na baadaye Waturuki, walichangia kwa kiasi kikubwa kueneza Uislamu katika Afrika Mashariki kwa ujumla, na hususan nchini Uganda kupitia Ufalme wa Buganda, ambao ndiyo msingi wa ustaarabu wa Uganda.

Zaidi ya yote, Waturuki ni wal-inzi, marafiki na waungaji mkono wa kihistoria wa Afrika Mashariki, na si maadui. Wakati wa utawala wa Dola ya Kiislamu ya Ottoman mwishoni mwa karne ya 16, Istanbul ilituma jeshi kupambana na ukoloni wa Wareno katika Afrika Mashariki. Kwa karne nyingi, jamii za Waislamu na Wasiokuwa Waislamu nchini Uganda ziliishi pamoja kwa amani na mshikamano, hadi walivyowasili Wakoloni wa Magharibi Makatili katika nusu ya pili ya karne ya 19. Kampuni ya Kibepari ya Kisingereza ya "Imperial British East Africa Company" ilitwaa na kuikwapua Uganda na kudhoofisha Dola ya Buganda kwa kuwaondoa viongozi Waislamu madarakani na kuwaweka watawala Wakristo waliokubaliana na kushirikiana na wakoloni hao. Tangu kipindi hicho hadi leo, Waislamu katika nchini ya Uganda wamekabiliwa na aina mbalimbali za ukandamizaji, ubaguzi na mate-so.

Mhariri

01 Rabiul Thani 1448 Hijria

Oktoba 2026 M

jukwalakhilafah@gmail.com

na mwanzoni mwa karne ya 20 CE dunia imeshuhudia vita zaidi ya 1200 na machafuko makubwa ya-siyohesabika yaliyogharimu mai-sha, rasilmali watu na vitu.

Vingi katika vita hivi ikiwa ni vya kupinga ukoloni na vita vya ki-maslahi ya wakoloni kama ilivyokuwa Vita Kuu ya Kwanza na ya Pili ya ulimwengu kati ya miaka ya 1914 mpaka 1918 na 1939 mpaka 1945.

Taarifa zinasema tangu mwaka 1900 vita ndani ya ulimwengu zimesababisha vifo vya watu zaidi milioni 187. Hii ni zaidi ya mara tatu ya watu wote wa nchi kama Tanzania, kwa sasa, na bado wanaendelea kusababisha vita zaidi. Hii leo kama inavyoonekana maeneo mbalimbali ulimwenguni kama Iraq, Afghan, Yemen, Libya, Palestina, Somalia, Congo nk. Ubepari hauwezi kamwe kuleta amani duniani, kwani ni mfumo wa kin-yonyaji na ni maumbile ya mwana-damu anaponyonywa kupinga un-yonyaji husika. Hivyo, mabepari kwa kuwa hunyonya walimwengu, na watu dunia nzima hupinga un-yonyaji wao, na hii ndiyo sababu kubwa inyoleta vita, vurugu, machafuko, mauaji, na kukosekana kwa amani ya ulimwengu kiu-jumla.

Ubepari ulistawi baada ya Waislamu kuacha kutabikisha Uis-lamu wao kivitendo na hatimaye kupelekea kuanguka kwa dola ya Kiislamu duniani (Khilafah), kuanzia hapo ulimwengu ukaanza kukosa mlinzi wa amani yake na amani ya ulimwengu kwa jumla. Hivyo, ili kurejesha tena amani ya kweli ya ulimwengu tunapaswa kurejesha tena serikali ya

kiulimwengu ya Kiislamu (Khilafah) ambayo itasimamia haki, amani, na uadilifu katika dunia hii kwa Waislamu na walimwengu kwa jumla.

Makazi ...kutoka uk 1

Kama ilivyo katika mambo mengi ambayo Ubepari kama Mfumo unaotawala ulimwengu kwa sasa umeshindwa, hata katika hili suala la makazi pia Mfumo huu fisidifu wa kibinafsi usijali watu wala utu isipokuwa kwa matajiri wachache umethibitisha kushindwa. Makazi chini ya Ubepari yanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo makazi yasiyo rasmi na yasiyopangwa, kukosa huduma ya maji safi na mifumo bora ya usafi wa mazingira, makazi yaliyojengwa katika maeneo hatarishi, hasa maeneo yanayokumbwa na mafuriko, yameongezeka kwa asilimia 122, kukosekana huduma za usafiri wa umma, barabara, na umeme, nk

Mtazamo wa Kiislamu kuhusu makazi ni mpana na toshelezi. Uislamu umelazimisha makazi kuwa sehemu ya utulivu wa binadamu tofauti na Ubepari ambapo leo hii makazi yanakubwa na uporaji, uvamizi, mauaji, fujo, vurugu na kufanya makazi kuwa si sehemu ya utulivu kwa binadamu. Anasema Allah(SWT) katika Qur'an


وَاللّٰهُ جَعَلَ لَكُم مِّنْ بُيُوتِكُمْ سَكَنًا

“Na Mwenyezi Mungu amekufanyieni katika nyumba zenu mahali pa utulivu”

(Nahal 80).

Uislamu pia umesisitiza juu ya makazi bora yenye stara na nafasi, amesema Mtume(SAW) “Mambo manne ni miongoni mwa sababu za furaha: mke mwema, nyumba bora yenye nafasi, jirani mwema, na chombo kizuri cha usafiri.”(Ibn Hibban).

Katika zama zote za Dola ya Kiislamu kwa takribani karne 13, ulimwengu ulishuhudia makazi bora na ukuaji wa miji mkubwa ya Kiislamu iliyopangwa vizuri na yenye huduma za kijamii Kwa watu wote na si kwa matajiri wachache pekee. Miji kama Baghdad, Cairo, Istanbul, Samarkand, Cordoba, nk ilishuhudia ukuaji ulioambatana na utulivu wa kijamii, ukuaji wa uchumi, ulinzi wa mazingira, na upatikanaji wa huduma za kijamii Kwa watu wote.



KUDHAMINI DENI PAMOJA NA FIDIA

Swali:

Assalamu Alaikum...

Swali hili ni la dharura. Mtu anadaiwa kiwango kikubwa cha pesa na kikundi cha wafanyabiashara. Mtu mwingine akajitolea kujadiliana na wafanyabiashara hao kuharakisha ulipaji wa haki zao (kabla ya muda wa malipo kufika) kutoka mfukoni mwake kwa sharti la kupunguzwa kwa thamani ya deni hilo. Kiasi kitakacho punguzwa hatimaye kitagawanywa, kwa kutolewa asilimia fulani, baina yake yeye mpatanishi na mwenye kudaiwa, yaani, kiwango kitakacho punguzwa kitakagawanywa baina ya mpatanishi na mwenye kudaiwa. Je hili linaruhusiwa? Allah akubariki na akusaidie katika mambo yako yote.

Jibu:

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullah Wa Barakatuhu

Naelewa kutokana na swali lako kuwa unadaiwa na wafanyabiashara, na kwamba kuna mtu anataka kukusaidia kulipa deni hilo kwa wafanyabiashara hao kwa niaba yako, lakini ameweka sharti kuwa atakubaliana na wafanyabiashara hao kupunguza thamani ya deni hilo, na kuchukua sehemu ya kiwango hicho kilicho punguzwa, kwa mfano ikiwa deni ni 10,000, atajadiliana nao walifanye kuwa 8,000, na anataka kuchukua 1000 kutoka kwako, kwa mfano, yaani, nusu ya kiwango kilicho punguzwa kama fidia ya kulipa kwake deni hilo kwa niaba yako. Kwa maana nyengine, anataka kuwa mdhamini wako kwamba utalipa deni hilo, kwa hivyo analilipa kwa niaba yako kwa mkabala wa fidia kutoka kwako, ambayo ni asilimia ya



kiwango kilicho punguzwa atakacho kipata kutoka kwa wafanyabiashara hao.

Ikiwa ufahamu wangu ni sahihi, muamala huu haujuzu kwa sababu uhalisia wake ni mkataba wa dhamana (Ad-Dhamana) ambayo ni kudhamini malipo ya deni kwa niaba yako, na dhamana katika Uislamu ina masharti. Moja ya masharti haya ni kuwa dhamana haijuzu kuwa na fidia. Lakini katika hali yako, anataka kuwa mdhamini wako kwa mkabala wa fidia. Muamala huu katika hali hii haujuzu. Dalili ya dhamana yafafanua wazi wazi kuwa kuna uunganishaji wa dhima kwa dhima, na kwamba ni dhamana ya kudumisha haki ya dhima. Na iko wazi kuwa kuna mdhamini, mdhaminiwa, na mwenye kudhaminiwa kwa ajili yake. Ni wazi kuwa haihusishi mkabala wa chochote (fidia). Dalili hii ni yale yaliyo simuliwa na Abu Dawood kutoka kwa Jabir kwamba amesema:

«كَانَ رَسُولُ اللَّهِ لَا يَصْلِي عَلَى رَجُلٍ مَاتَ وَعَلَيْهِ دَيْنٌ قَائٍ بِمَيْتٍ فَقَالَ عَلَيْهِ دَيْنٌ قَالُوا نَعَمْ دِينَارَانِ قَالَ صَلُّوا عَلَى صَاحِبِكُمْ فَقَالَ أَبُو قَتَادَةَ الْأَنْصَارِيُّ هُمَا عَلَيَّ يَا رَسُولَ اللَّهِ قَالَ فَصَلَّى عَلَيْهِ رَسُولُ اللَّهِ e فَلَمَّا فَتَحَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ r قَالَ أَنَا أَوَّلُ بِكُلِّ مُؤْمِنٍ مِنْ نَفْسِهِ فَمَنْ تَرَكَ دَيْنًا فَعَلَيْ قَضَاؤُهُ وَمَنْ تَرَكَ مَالًا فَلِرِوَاتِهِ».

“Alikuwa Mtume (saw) hamswalii mtu yeyote aliye kufa na huku ana deni juu yake. Ikaletwa maiti akauliza: Je, ana deni juu yake? (Watu) wakasema:

ndiyo, dinar mbili. Akasema: mswalieni mwenzenu. Kisha Abu Qatadah al-Ansari akasema: dinar mbili hizo zitakuwa juu yangu ewe Mtume wa Allah. Mtume wa Allah (saw) akamswalia. Na pindi Allah alipomfungulia Mtume wake (saw), alisema: mimi ni aula kwa kila muumini kuliko nafsi yake, yeyote atakaye acha deni basi litakuwa juu yangu kulilipa na yeyote atakaye acha mali basi itakuwa ya warathi wake.”

Ni wazi katika Hadith hii kuwa Abu Qatada amejumuisha dhima yake na dhima ya maiti katika jukumu la haki ya kifedha anayodai mkopesheji. Ni wazi kuwa dhamana hii inajumuisha mdhamini, mwenye kudhaminiwa, na wenye kudhaminiwa kwa ajili yake, na kwamba, dhamana ambayo wote wamekubaliana kwayo, inajifunga juu ya haki ya dhima pasi kuwepo mkabala (fidia). Hadith hii imejumuisha masharti ya uhalali wa dhamana, na vipengee vya mkataba wake.

Hivyo basi, katika hali yako inajuzu kwa mtu huyo kuwa mdhamini wako kukulipia deni lako, na inajuzu kwake kukubaliana nawe (mwenye deni), lakini haijuzu kuchukua chochote kama mkabala, kwa hivyo haijuzu kwake kutaka chochote kama mkabala.

Allah ni Mjuzi

Ndugu yenu Atta Ibn Khalil Abu Al-Rashtah

Amiri wa Hizb ut Tahrir

Tarehe 17 Rabiul-Thani 132H ilianguka Khilafah ya Bani Ummayah, Khilafah iliyotawala ulimwengu kwa takribani miaka 91, yaani kuanzia mwaka 41H (661M) mpaka mwaka 132H(750M).

Utawala wa Bani Ummayah ulianza kwa Muawiya Ibn Abu Sufiani, maarufu kama Muawiya(I) na kumalizikia kwa Marwan ibn Muhammad ibn Marwan maarufu kama Marwan(ii) ikiwa na jumla ya makhalifah 14.

Imeitwa Khilafah ya Bani Ummayah kwa sababu Makhalifah wake wanatokana na ukoo wa Kiqureshi wa Bani Ummayah ambao unatokana na Umayya ibn Abd Shams ambaye ni baba yake na Abu Sufiani Swaghir Ibn Harb na babu yake na Muawiyah-Muawiyah Ibn Abu Sufiani. Makao makuu ya dola hii yalikuwa Sham (Damascus/Syria). Kupitia Khilafah hii ya Banu Ummayah, ummah wa Kiislamu unaweza kujifunza mambo mengi kama ifuatavyo: Ummah wa Kiislamu ni lazima uwe na kiongozi mmoja, Khalifah wa Waislamu wote ulimwenguni. Baada ya kumalizikia kwa Khilafah bora (Khilafah Rashidah) iliyodumu kwa miaka 30 kuanzia mwaka 11H mpaka mwaka wa 41H ikiwa na jumla ya makhalifah 4 ambao ni Abuobakr, Umar, Uthman na Ally Allah awaridhie, Banu Ummayah waliendeleza utawala wa Kiislamu ili kutabikisha sheria za Muumba katika ardhi.

Kwahiyo masahaba kama ambavyo hawakukubali kuishi



bila uongozi wa Kiislamu baada ya kufariki kwa Mtume (SAW) pia hawakukubali kuishi bila ya uongozi wa Kiislamu baada ya Khilafah bora kwani bila uongozi hakuna utabikishwaji wa hukumu na sheria za Kiislamu na kuridhia kutabikisha hukmu zisizokuwa za Kiislamu ni ukafiri wa wazi. Allah (SWT) anasema:

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ (٤٤)

“Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri”

Kupitia Khilafah ya Bani Ummayah tunajifunza kuwa sifa ya serikali ya Kiislamu na mfumo wa Uislamu ni kujitanua kupitia da’awah na jihad. Katika kipindi cha Khilafah bora (Rashidun) eneo la dola ya Kiislamu lilikuwa takriban 6,400,000 km² lakini chini ya Banu Ummayah eneo la Khilafah liliongezeka na kufikia takribani 11,100,000 km².

Khilafah ya Bani Ummayah ilitawala Mashariki ya kati, Asia ya magharibi, Asia ya kati ambayo kwa sasa ni nchi za Uzbekistan, Tajikistan, Kazakhstan, Turkmenistan, Afghanistan na Kyrgyzstan, Afrika ya kaskazini na Kaskazini Magharibi, magharibi ya China na baadhi ya sehemu ya Ulaya kama vile Hispania na Ulaya ya Mashariki. Hii ni kutekeleza maarisho ya Mtume (SAW)

عَنِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((أَمَرْتُ أَنْ أَقَاتِلَ النَّاسَ حَتَّى يَشْهَدُوا أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ، وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ، فَإِذَا فَعَلُوا ذَلِكَ عَصَمُوا مِنِّي دِمَاءَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ إِلَّا بِحَقِّ الْإِسْلَامِ، وَحِسَابُهُمْ عَلَى اللَّهِ تَعَالَى)) رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ وَمُسْلِمٌ

Imepokelewa kutoka kwa Ibn ‘Umar (RA) kwamba Mtume (SAW) amesema:

“Nimeamrisha nipigane vita na watu mpaka washahidie kwamba hakuna anayepaswa kuabudiwa kwa haki ila Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah, na wasimamishe Swalaah na watoe Zakaah. Watakapofanya hivyo, watakuwa wamepata ulinzi kwangu wa damu zao, na mali zao isipokuwa kwa haki ya Uislamu, na hesabu yao itakuwa kwa Allaah Ta’aalaa.” (Bukhaariy & Muslim)

Khilafah hii pia inatufundisha uadilifu wa hali ya juu wa serikali ya Kiislamu. Katika utawala wa Khalifah wa 6 wa Khilafah ya Bani Ummayah, Al-Walid ibn Abd al-Malik ibn Marwan, maarufu kama Al-Walid(I), Waislamu waliingia Asia ya kati katika Samarkand ambayo ni Uzbekistan ya leo, mwaka wa 83H. Kamanda wa jeshi la Waislamu, Qutaybah Ibn Muslim aliwapiga vita vita watu wa Samarkand na kuwatala bila kiwalingania kwanza.

Watu wa Samarkand walishtakia suala hili kwa Khalifah na mara baada ya kusikilizwa kesi, ilihukumwa kuwa Waislamu wamekosea na waondoke Samarkand mara moja. Wakati

Inaendelea uk 6

Waislamu wanaondoka watu wa Samarkand wakawarudisha na kukubali kutawaliwa na Uislamu. Qadhi aliyesimamia kesi hii alikuwa Umar Ibn Abdulaziz, kabla hajawa Khalifah. (Ally Tantawi: Qasas Min Al Tarikh UK 85)

Pia tunajifunza kuwa Uislamu si dini ya kiroho pekee bali ni mfumo kamili wa maisha ya binadamu ulio na masuluhisho kamili ya matatizo yote ya binadamu kiitika-di, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika kipindi Khilafah ya Bani Umayyah hususani katika utawala wa Khalifah wa 8 aliyetawala kuanzia mwaka wa 99H, Khalifah Umar Ibn Abdulaziz, dola ya Kiislamu ilifanikiwa kuondoa umasikini kwa kiasi kikubwa.

Anasimulia Yahya Ibn Said, aliyekuwa Wali (governor) wa Afrika Kaskazini katika kipindi cha utawala wa Khalifah Umar Ibn Abdul Aziz, anasema: “nilitumwa na Umar Ibn Abdul Aziz kukusanya zakat Afrika. Baada ya kukusanya nilikusudia kuzigawa kwa masikini. Lakini sikupata masikini wa kumpa, Umar Ibn Abdul Aziz alimfanya kila mtu kuwa tajiri katika kipindi cha utawala wake. Mwisho, niliamua kutumia pesa hizo za zakat kununua watumwa na kuwaacha huru” (Ibn Abd Hakam, Abdullah (1994) Al Khilafat Al Adil Umar Ibn Abdul Aziz: Khamis Al Khulafah Al Rashidin, Dar Al Fadilat)

Hakika ya kujifunza katika Khilafah hii ni mengi lakini muhimu kabisa ni kuwa ilikuwa Khilafah, ilikuwa utawala wa Kiislamu wa kiulimwengu ambao hauna budi isipokuwa kuwepo. Ni wajibu wetu kama Waislamu kufanya

kazi kurejesha utawala wa Kiislamu ulimwengu ili hatimaye Uislamu utabikishwe kivitendo kamili kama dini na mfumo kamili wa maisha ya mwanadamu.

Kwa kufanya hivi huenda Allah (SWT) akaturidhia nasi tunamuomba Allah tuwe miongoni mwa waliofatimiza ahadi ya Allah na bishara ya Mtume (SAW) alipotuambia:

ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَىٰ مِنْهَاجِ النَّبِيِّ ثُمَّ سَكَتَ

“Kisha itarejea Khilafah kwa njia ya Mtume” (Ahmad)

BAADHI YAMATUKIO YA MWEZI OKTOBA

- 1/10 Siku ya Wazee Duniani
- 5/10 Siku ya Walimu Duniani
- 7/10 Siku ya Makaazi Duniani
- 10/10 Siku ya Kukomeshwa Adhabu ya Kifo
- 10/10 Siku ya Magonjwa ya Akili
- 14/10 Siku ya Kumbu Kumbu ya Nyerere
- 16/10 Siku ya Chakula Duniani
- 17/10 Siku ya Kupambana na Umasikini
- 20/10 Siku ya Mashujaa Kenya
- 24/10 Siku ya Umoja wa Mataifa (UN)
- 25/10 Kumalizika Vita baina ya Waarabu na Israel- 1973

BAADHI YAMATUKIO YA MWEZI RABI-UL THANI

1. Vita vya Bahrain

Mtume Saaw aliongoza doria kubwa ya kiasi cha kikosi cha askari 300 katika mji wa Bahrain. Haku-kutokea mapigano yoyote. (Mwaka wa 3AH.)

2. Kutumwa kikosi cha Abuu Ubeida Ibn Jarrah

Mtume SAAW alituma kikosi hiki cha watu 40 kuelekea Dhi al-Qiswa kwa Bani Thaalabah, baada ya kuuwawa wenzake Muhammad bin Maslamah. Maadui wakashambuliwa na kushindwa. (Mwaka wa 6 AH)

3. Kutumwa kikosi cha Zaid bin Harithah

Kilitumwa katika mji wa Al Jumumu kwa Bani Saleem. Kwa msaada wa mwanamke wa Bani Muzaina Waislamu waliweza kushinda kiurahisi (6AH)

Jemadari mkubwa wa Kiislamu Khalid bin al-Walid afariki dunia Mwaka 21 Hijria

Kuanza Vita vya Jamal ndogo (25 Rabiul-thani- Mwaka wa 36 AH.)

Kujiuzulu Uongozi kwa Khalifa wa tatu wa Bani Umayyah ya Mu'awiya bin Yazid (Muawiyah II) Mwaka 64 Hijria (Disemba 21, 683 miladi)

Siku ya tarehe 17 Septemba 1978 ilikuwa ni siku ya msiba, majonzi kufuatia usaliti wa Raisi Saadat wa Misri kufikia makubaliano ya Camp David na kijidola cha Mayahudi. Makubaliano hayo yalijiri baada ya Vita vya Harb ur Ramadhan / Yom Kippur vilivyopiganwa mwaka 1973 (Oktoba 6 – 25) vilikhusisha muungano wa nchi za Kiarabu chini ya uongozi wa Misri na Syria dhidi ya Israel.

Itakumbukwa kwamba vita vyote wanavyopigana vibaraka wa nchi za kiarabu dhidi ya kijidola cha Israel ni vita vya kisani vikiwa na malengo maalumu na kamwe sio kuiondoa dola hiyo. Vita vya Siku Sita vya mwaka 1967 baina ya Israel na waarabu vilibuniwa na Uingereza kama jaribio la maksudi kuidhoofisha athari ya Marekani kwa kumdhoofisha kibaraka wake mwenye nguvu Jamal Abdel Nasser wa Misri. Israel ilitumika kama mdau mkuu ikiwa na tamaa ya fisi ya kupata ardhi ziwe kama chambo katika mazungumzo na nchi za kiarabu na kujionesha kwa ulimwengu hususan wa Kiislamu kama ni nchi isiyoshindika! (invincible)

Israel ikapiga katika Juni 5-1967 na kuangamiza kiasi cha jeshi la Misri na kuathiri pia majeshi ya Syria na Jordan. Kadhalika ikashikilia maeneo nyeti ya Sharm-al Sheikh na Ukanda wa Tiran (Misri), Ukanda wa Magharibi (Jordan) na Milima ya Golan ya Syria. Lengo la vita likafikiwa kumdhoofisha Nasser, kuimakinisha Israel kwa kuipatia ardhi ili kufanikisha mazungumzo ya amani katika



mustakbal.

Vita vya 'Harb-ur-Ramadhan (Vita vya Ramadhan/ Yom kippur) vya mwaka 1973 vilivyopiganwa ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani viliasisiwa na Raisi Saadat baada ya kufariki Raisi Nasser akishirikiana na Raisi Assad wa Syria sio kwa lengo la kuangamiza Israel bali kwa dhamira ya kuzijenga haiba zao, kwa kuwa walikuwa watawala wapya, kuipa nguvu Israel na kuandaa mazingira ya kufanya mazungumzo na kijidola hicho cha mayahudi. Yote haya chini ya maelekezo ya Marekani kwa kuwa watawala hawa walikuwa ni vibaraka wake watiifu.

Vita hivi Waislamu waliitikia Jihadi katika hali ya ajabu kabisa! kiasi cha kushiriki maelfu ya wanamgambo kwa kuwa inaruhusiwa kupigana jihadi hata chini ya kiongozi dhalim. Na majeshi yalipigana kwa ujasiri mkubwa, katika masaa 24 kuanzia oktoba 6 walidiriki kuivunja ngome ya mayahudi ya Bar-leva ilhali Waislamu wakipoteza askari wachache tu. Syria ilituma vifaru 500 katika Milima ya Golan na kukomboa baadhi ya ardhi zilizochukuliwa mwaka 1967. Kwa kipindi cha siku mbili Israel ilipoteza ndege 49 na vifaru 500 na ilishindwa vibaya na kutapatapa kwa karibu wiki tatu.

Ghafla katika hali isiyo ya kutarajia kati kati ya mapigano Raisi Saadat alituma ujumbe kwa Kissinger, Waziri wa Nje wa Marekani kutaka

sulhu na mayahudi. Mwezi wa Novemba 1977 Saadat alilihutubia Bunge la Israel, na mwaka 1978 kufikia mawafikiano ya Mkataba wa 'Camp David'. Katika mwaka 1981 akatiliana mkataba rasmi na mayahudi. Mkataba wa kuipa nguvu na kuitambua dola hiyo ambayo haiajawahi kusita kuuwa na kudhalilisha Waislamu.

Tukiwaangalia viongozi katika nchi za Kiislamu hatuoni zaidi ya dhulma, khiyana na usaliti kinyume na tunavyowaona Makhalifa wetu watukufu katika tareekh yetu tukufu ya Kiislamu. Kwa hakika, Umma wa Kiislamu una kiu ya viongozi majasiri na wenye ikhlasi ambao leo kwa msiba mkubwa imekuwa bidhaa adimu katika biladi zetu. Jukumu letu ni kufanya kazi ya kurejesha tena Khilafah ili tuweze kupata viongozi ambao tutaweza kujifakharisha kwa ukweli na uchamungu wao.

PICHA ZA TUKIO LA SEMINA

SEMINA: UISLAMU NA MAADILI

MAADILI MABAYA



Mavazi ya Ovyo

MAADILI MEMA YA UISLAMU



Uaminifu na Uadilifu



Wema na Huruma



Hizb ut Tahrir
Tanzania

f X i S W Hizb ut Tahrir Tanzania / hizbtz.org

